



WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI (TARURA)

TAARIFA KWA UMMA

USIMAMIZI NA UDHIBITI WA BARABARA ZA WILAYA (DISTRICT ROADS)

Kanuni Na 30(1)(a) ya Usimamizi wa Barabara, 2009 chini ya Sheria ya Barabara, 2007

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ni Wakala katika Wizara chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali Sura Namba 245 na kutangazwa rasmi kwenye gazeti la Serikali Na 211 la tarehe 12 Mei 2017. Wakala umechukua majukumu ya utekelezaji kuhusiana na ujenzi na matengenezo ya mtandao wa barabara za Vijijini na Mijini ambayo hapo awali yalikuwa yakitekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Jukumu kubwa la Wakala ni usimamizi, ujenzi, na matengenezo ya mtandao wa barabara za vijijini na mijini ikijumuisha kuimarisha usalama wa barabara, kulinda hifadhi za barabara zisivamiwe na kudhibiti athari za mazingira na za kijamii.

Pamoja na kuimarisha usalama na kulinda hifadhi za barabara, pia Wakala una jukumu la kuzilinda barabara zisiharibike mapema kwa kudhibiti uzito wa magari pamoja na urefu, upana na kina kwa kuzingatia Kanuni Namba 4 ya Kanuni za Usalama Barabarani (Uzito wa juu wa Vyombo vya moto/magari) za 2001 “The Road Traffic (Maximum Weight of Vehicles) Regulations 2001” chini ya Sheria ya Usalama barabarani Sura 168 vikisomwa kwa pamoja na Kifungu Namba 42 (3) cha Sheria ya Barabara Na. 13 ya 2007 “The Roads Act, 2007”.

Tunawakumbusha wasafirishaji kuzingatia ukomo wa uzito uliooneshwa katika vibao vya alama za barabarani wakati wanaposafirisha mizigo kupitia katika barabara zetu na pia kutovamia hifadhi za barabara.

Pia katika kutekeleza majukumu yake, Wakala una vyanzo vya fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa kwenye hati ya uanzishwaji wa Wakala ya mwaka 2017 '*The Executive Agencies(Tanzania Rural and Urban Roads Agency) Establishment Order, 2017*' ambavyo ni fedha toka Serikali kuu, fedha toka Bodi ya Mfuko wa Barabara, mikopo na misaada toka kwa wadau wa maendeleo (Development Partners), ada ya maegesho ya magari kwenye hifadhi za barabara, ada ya matumizi ya hifadhi za barabara nk..

Hivyo TARURA ina jukumu pia la kutoza ada kwa maegesho ya magari katika hifadhi ya barabara na matumizi ya hifadhi ya barabara (kwa mfano kupitisha 'cable' za mawasiliano) ikiwa ni pamoja na kusimamia matumizi ya hifadhi za barabara.

Aidha, tunawajulisha wananchi kuwa TARURA haihusiki kwa namna yoyote na utozaji wa tozo zilizokuwa zikitozwa na Mamlaka zingine hapo awali kwa Malori na Makontena kuingia katikati ya majiji na Manispaa kwa kupitia sheria zao.

TARURA wajibu wake ni kusimamia na kudhibiti matumizi ya barabara zake zisiharibike kabla ya muda uliokusudiwa, kulinda uvamizi wa hifadhi za barabara, na kuimarisha usalama katika barabara zake kwa kuzingatia sheria nilizozitaja hapo juu.

Imetolewa na:

**MTENDAJI MKUU
TARURA - DODOMA
6 December 2018**